BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SITA

Kikao cha Tano – Tarehe 16 Mei, 2017.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa Mwaka 2017/2018.

Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa Mwaka 2017/2018.

II. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

126. MHESHIMIWA ABDALLA MAULID DIWANI (Jimbo la Jang'ombe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Tunaipongeza sana Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kutekeleza miradi ya TASAF inayokusudia kuwaondolea shida ya maji wananchi wetu wa sehemu mbali mbali kwa kuchimba visima katika maeneo hayo. Hata hivyo, kumetokea kero ya kulipishwa gharama kwa wananchi wa sehemu husika zenye visima hivyo pindi linapotokea tatizo.

(a) Je, Serikali inalitambua suala hili la ZAWA kuwalipisha wananchi matengenezo ya visima vilivyochimbwa kupitia miradi ya TASAF.

(b) Je, ni Sheria gani inayowataka wananchi walipie gharama za ukarabati wa visima hivyo.

(c) Je, Serikali imechukua hatua gani katika kukabiliana na tatizo la wananchi kulipishwa gharama za matengenezo ya visima hivyo.

.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

117. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

Kwa kuwa kwa sasa kuna zoezi la uajiri wa wafanyakazi wa kada tofauti za Afya. Na kwa kuwa agizo la Serikali linamtaka mfanyakazi aombe kituo maalumu atakachofanya kazi ili kuepusha kuhamishwa kiholela kwa wafanyakazi. Kwa sasa inaonekana kwamba vijana wengi huomba nafasi za kazi kutoka Pemba lakini baada ya muda mfupi wa kuajiriwa huomba uhamisho ili waje kufanyakazi Unguja kwa visingizio tofauti.

(a) Je, kwenye zoezi la uajiri kwa Wizara ya Afya, umezingatiwa muongozo huo wa mtu kupangiwa kazi katika kituo alichoomba na kwa muda maalum.

(b) Je, Tume ya Utumishi ina mpango wa kuusimamia mpango huo ili kuondoa manung'uniko kwamba waajiriwa wengi wanaofanya kazi Pemba ni vijana wanatokea Unguja na baada ya muda mfupi huomba uhamisho na kuviacha vituo vyao vya kazi vikiwa na upungufu mkubwa wa wafanyakazi.

Waziri wa Fedha na Mipango:

62. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Waziri wa Fedha na Mipango:

Ni wafanyakazi wangapi kutoka Zanzibar walioajiriwa katika Benki Kuu ya Tanzania.

Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko:

26. MHESHIMIWA MWANAIDI KASSIM MUSSA (Nafasi za Wanawake) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko:

Kama tunavyofahamu zao la Karafuu ni zao kuu linalotegemewa na Serikali yetu.

(a) Je, pamoja na mipango mizuri iliyopangwa kuhusu wananchi wetu kuwekewa mazingira mazuri ya kuchuma karafuu hadi kufikia kuuza, Wizara yako ina mpango gani wa kuwakopesha pesa wakulima wa zao hili ili kufanikisha zaidi uchumaji huo.

(b) Je, wale wanaopata mkopo na baada ya uchumaji wa karafuu kuamua kutoziuza karafuu hizo Serikalini na kuuza maeneo mengine, huwa wanachukuliwa hatua gani.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

33 MHESHIMIWA TATU MOHAMED USSI (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto:

Kama tunavyojuwa kuwa Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto inatoa mikopo kwa vikundi mbali mbali vikiwemo vya Wajasiriamali ambao hawajajiunga na vikundi vya Ushirika.

(a) Je, ni vikundi vingapi Unguja na Pemba ambavyo vimepewa mikopo kwa mwaka wa 2015-2016.

(b) Wajasiriamali mmoja mmoja wangapi ambao wamepewa mikopo Unguja na Pemba kwa ajili ya kujipunguzia makali ya umasikini.

Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

128. MHESHIMIWA SULEIMAN MAKAME ALI (Jimbo la Ziwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira:

Mnamo mwaka 1982 Serikali kupitia Shirika la Umeme ilipitisha laini kubwa ya umeme yaani “HIGH TENSION” iliyotoka Wesha kwenda Tibirinzi kupitia kwenye makaazi ya wananchi wa maeneo ya Mshangama Shehia ya Wesha. Hata hivyo, hadi leo wananchi wa maeneo hayo hawajapatiwa fidia na wanaendelea kuishi katika sehemu hizo hatarishi.

Je, ni lini wananchi hao watalipwa fidia ili waweze kuondoka katika maeneo hayo hatarishi.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

36. MHESHIMIWA SHAIBU SAID ALI (Jimbo la Chonga) - Atamuuliza Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Kuna njia zilizojengwa kwa majaribio kisiwani Pemba kama vile Chanjaani – Pujini, Chanjamjawiri – Tundaua, Mizingani – Wambaa na kadhalika. Lakini njia hizo hivi sasa zinaendelea kuharibika kwa kasi sana, na baada ya muda mfupi ujao barabara hizo zinaweza kurudia hali mbaya kama zilivyokuwa kabla ya ujenzi huo.

(a) Je, Wizara ina utaratibu gani wa kuzifanyia ukarabati njia hizo ili zisiendelee kuharibika zaidi.

(b) Kama njia hizo zilikuwa kwenye majaribio, Je Wizara imeridhika na kiwango cha njia hizo.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka 2017/2018.

Waziri wa Nchi, (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum kwa Mwaka 2017/2018.

`

Zanzibar,
16 Mei, 2017.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.